JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA

MFUKO WA PEMBEJEO

MKURUGENZI MTENDAJI MFUKO WA PEMBEJEO
S.L.P. 32081
DAR ES SALAAM

Simu: 022 2700191
Fax: 022 2700191

Barua pepe:
agitf@mari.or.tz au agitf@pkilimo,go.tz au executive@mari.or.tz

WIZARA YA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA

MFUKO WA PEMBEJEO

Mfuko wa Pembejeo unatoa mikopo mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji katika sekta ya kilimo na mifugo. Mikopo hiyo ni pamoja na ya pembejeo, ununuzi wa matrekta mapya, mikopo ya kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta na kukarabati matrekta, mikopo ya kununua matrekta madogo ya mkono (Power tillers), zana za kukokotwa na ng'ombe kama vile plau, zana ndogo ndogo za umwagiliaji kama vile pampu, mashine ndogo ndogo za kusindika na kuongeza thamani ya mazao. Zifuatazo ni taratibu za kuomba mikopo hiyo.

1. MIKOPO YA PEMBEJEO ZA KILIMO NA MIFUGO

Walengwa wa mikopo ya pembejeo za kilimo na mifugo ni wakulima au wafugaji kupitia kwenye vikundi, wakulima au wafugaji binafsi, Vyama vya Msingi, Mifuko ya Pembejeo ya Wilaya, Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) na mawakala wa pembejeo wenye uzoefu usioupungua miaka miwili.

Pembejeo zinazoweza kuombewa mikopo ni rnbolea za aina mbalimbali za viwandani, mbegu bora, dawa za tiba na chanjo za mifugo, vyakula vya mifugo, dawa za kuhifadhi mazao ya kilimo na mifugo, vifungashi vya mazao ya kilimo na mifugo na sumu za magugu.

A) Uteuzi wa waombaji-mikopo ya Pembejeo za kilimo na Mifugo

- Halmashauri za Wilaya zitatoa tangazo la kuwapo mikopo ya pembejeo za kilimo na mifugo kupitia Mfuko Pembejeo

- Waombaji watatakiwa kujaza fomu maalum za maombi na kutoa maelezo binafsi, anuani ya makazi na biashara/shamba ikiambatanishwa na mchanganuo wa matumizi ya mkopo anaoomba (Business plan), kivuli cha leseni hai ya biashara ya pembejeo kwa wafanya biashara na kivuli cha hati ya dhamana ambacho mmiliki wake ndiye anayeomba mkopo.

- Maafisa Kilimo/Mifugo wa Wilaya watathibitisha shughuli zinazoombewa mikopo katika wilaya husika. Fornu za maombi zitahakikiwa na kusainiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya na Afisa Kilimo/Mifugo Wilaya.

- Fomu za maombi ya mikopo ziwasilishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya katika muda maalum kama ifuatavyo

- **Machi hadi Mei,** mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Iringa, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Kigoma, Kagera, Mara na Mwanza.

-Agosti hadi Septemba, mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Pwani, Mtwara, Lindi Dar es salaam.

Fomu za maombi na vielelezo vinavyohitajika pamoja na mahitaji ya pembejeo ya wilaya husika zitatumwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Pembejeo.

Maombi haya huchambuliwa na kuwasilishwa kwenye kikao cha Bodi ya Wadhamini wa Mfuko ili yaidhinishwe. Maamuzi ya Bodi hutumwa kwa waombaji na kwenye Halmashauri za Wilaya huska.

B) Masharti ya Mikopo ya Pembejeo za Kilimo na Mifugo

- Wauza pembejeo binafsi, wakulima na wafugaji kupitia kwenye vikundi au wakulima na wafugaji binafsi sharti wawe na dhamana isiyohamishika yenye hati miliki (Title deed) na inayokubalika kisheria. Mwombaji sharti awe ndiye mmiliki wa hati itakayodhamini mkopo.

- Mwombaji awe amefanya biashara ya pembejeo kwa muda usiopungua miaka miwili.

- Mifuko ya Pembejeo ya Wilaya isiyo na dhamana zenye hati miliki itadhaminiwa na Halmashauri za Wilaya husika.

- Vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS), vikundi vya wakulima na wafugaji visivyo na dhamana za hati miliki sharti viwe na akiba ambayo ni sawa na theluthi moja ya mkopo wanaoomba. Waombaji wa kundi hili watatakiwa kuwa wanachama wa asasi ya kifedha itakayotoa mkopo kwa niaba ya Mfuko wa pembejeo.

- Muda wa mkopo ni miezi kumi na nane kwa riba ya asilimia nane (8%).

2. MIKOPO YA KUNUNUA TREKTA MPYA

Walengwa wa mikopo hii ni wakulima binafsi wanaomiliki mashamba yenye ukubwa usiopungua ekari hamsini.

A) Uteuzi wa waombaji wa mikopo ya kununulia matrekta mapya

- Halmashuri za Wilaya zitatoa tangazo kuhusu kuwepo kwa mikopo ya ununuzi wa matrekta mapya kupitia Mfuko wa Pembejeo.

- Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya maombi itakayopitishwa na Afisa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Mji au Manispaa husika

- Maombi yote yatatumwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Pembejeo.

- Mfuko wa Pembejeo utachambua maombi na kuyawasilisha kwenye Bodi ya Wadhamini wa Mfuko.

- Maombi haya huchambuliwa na kuwasilishwa kwenye kikao cha Bodi ya Wadhamini wa Mfuko ili yaidhinishwe. Maamuzi ya Bodi hutumwa kwa waombaji na kwenye Halmashauri za Wilaya husika.

B) Masharti ya Mikopo ya Kununua Trekta

- Mwombaji sharti awe na dhamana isiyohamishika yenye hati miliki (Title deed) na inayokubalika kisheria ambayo mwombaji ndiye mmiliki wake.

- Mwombaji sharti awe na shamba lenye ukubwa usio chini ya ekari 50 na awe tayari kutoa huduma na kukodisha trekta hilo kwa wakulima wenzake

- Mwombaji atatakiwa kulipia gharama za kutathmini dhamana ya mkopo wake pamoja na asilimia moja ya mkopo utakaokuwa umeidhinishwa.

- Mwombaji atatakiwa kulifanyia matengenezo madogo na makubwa trekta litakalonunuliwa kwa mkopo mara kwa mara kama atakavyoelekezwa na mtengenezaji au muuzaji wa trekta hilo. Aidha, trekta hilo litakuwa sehemu ya dhamana ya mikopo na kadi ya uandikishaji (Registration card) itakuwa chini ya umiliki wa Mfuko mpaka mkopo utakaporejeshwa.

- Mkopo wote na riba utatakiwa urejeshwe katika kipindi cha miaka mitatu- (3) kwa riba ya asilimia nane (8%) kwa miaka mitatu.

3. MIKOPO YA KUKARABATI TREKTA

Walengwa wa mikopo hii ni wamiliki wa matrekta ambayo yanaweza kukarabatiwa kwa gharama isiyozidi shilingi milioni tatu na laki tano.

A) Uteuzi wa waombaji wa Mkopo ya Kukarabati Trekta

- Halmashauri za Wilaya zitatoa matangazo kuhusu kuwepo kwa mikopo ya kukarabati matrekta kupitia Mfuko wa Pembejeo. Mwombaji sharti awe tayari kutoa huduma ya kukodisha trekta hilo kwa wakulima wenzake

- Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya maombi itakayopitishwa na Afisa Kilimo na Maendeleo ya

Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa.

- Maafisa Zana katika Halmashauri watashirikiana na mmiliki pamoja na fundi wake kufanya tathmini ya kiwango cha ubovu wa matrekta hayo katika maeneo yaliyoanishwa katika taarifa ya tafiti za awali na ukarabati. Mapendekezo yazingatie kiwango cha matengenezo ili gharama za vipuri na fundi zisizidi kiwango cha juu kinachoweza kutolewa.

- Maombi yote yatatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Mfuko wa Pembejeo baada ya kupitishwa na Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa husika.

- Mfuko wa Pembejeo utachambua maombi hayo kwa kuzingatia taarifa ya tathmini ya Maafisa Zana wa maeneo husika ikiwa ni pamoja na kuhakiki kuwepo kwa trekta zinazoombewa mkopo.

- Maombi haya huchambuliwa na kuwasilishwa kwenye kikao cha Bodi ya Wadhamini wa Mfuko ili yaidhinishwe. Maamuzi ya Bodi hutumwa kwa waombaji na kwenye Halmashauri za Wilaya huska.

B) Masharti ya Mikopo ya Kukarabati Trekta

*Dhamana ya mkopo ni hati miliki ya nyumba au shamba pamoja na kadi halisi ya trekta ambalo mmiliki wake ndiye atatakiwa kuomba.

- Mwombaji atawasilisha ankara vifani kutoka kwa muuzaji aliyeingia mkataba na Mfuko wa Pembejeo. Malipo yatafanyika moja kwa moja kwa muuzaji wa vipuri.

- Mwombaji atatakiwa kulipa asilimia moja ya mkopo utakaokuwa umeidhinishwa

- Muda wa mkopo ni miezi kumi na nane kwa riba ya asilimia nane (8%).

4. MIKOPO YA MATREKTA MADOGO YA MIKONO (POWER TILLERS)

Walengwa ni wakulima binafsi, vikundi vya wakulima hasa kwenye maeneo ya umwagiliaji vilivyosajiliwa kisheria, Vyama vya Msingi Mifuko ya Pembejeo ya Wilaya na Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS).

A) Uteuzi wa Waombaji wa Mkopo

- Halmashauri za Wilaya zitatoa matangazo kuhusu kuwepo kwa mikopo ya matrekta madogo ya mkono (Power tillers) kupitia Mfuko wa Pembejeo.

- Waombaji wa mikopo hii watatakiwa kujaza fomu za maombi zitakazopitishwa na Afisa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa husika.

- Maombi yote yatatumwa kwa Mkurugenzi Mtendaji Mfuko wa Pembejeo, pamoja na vielelezo vyote vitakavyokuwa vimeanishwa kwenye fomu ya maombi

- Mfuko wa Pembejeo utachambua maombi hayo na kuyawasilisha kwenye Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Pembejeo kwa ajili ya kuidhinishwa.

B) Masharti ya Mkopo

- Wakulima binafsi sharti wawe na dhamana isiyohamishika yenye hati miliki (Title deed) na inayokubalika kisheria.

- Mifuko ya Pembejeo ya Wilaya isiyo na dhamana zenye hati miliki sharti ipate udhamini wa Halmashauri za Wilaya husika

- Vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS), vikundi vya wakulima visivyo na dhamana za hati miliki sharti viwe wanachama wa Shirikisho la Vyama vya Kuweka na Kukopa Tanzania (SCCULT, 1992 Ltd.). Kiasi cha mkopo utakaotolewa ni mara tatu ya akiba ya mwombaji.

- Muda wa mkopo ni miaka mitano kwa riba ya mikopo ni asilimia nane (8%).

5. MIKOPO YA KUANZISHA VITUO WA KUKODISHA MATREKTA

Walengwa ni waombaji binafsi wenye uzoefu wa kutumia matrekta. Vituo vya kukodisha matrekta vitaanzishwa kwenye maeneo yenye mahitaji makubwa ya matrekta

A) Uteuzi wa Waombaji wa Mkopo

- Halmashauri za Wilaya zitatoa tangazo kuhusu kuwepo kwa mikopo ya kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta kupitia Mfuko wa Pembejeo. Vituo vitaanzishwa kwa kukopeshwa matrekta kati ya mawili hadi matano kulingana na thamani ya dhamana.

- Waombaji wa mikopo hii watatakiwa kujaza fomu ya maombi itakayopitishwa na Afisa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa husika.

- Maombi yote yatatumwa kwa Mkurugenzi Mtendaji Mfuko wa Pembejeo yakiwa na vielelezo vyote kama vitakavyokuwa vimeainishwa kwenye fomu ya maombi.
- Mfuko wa Pembejeo utachambua maombi hayo na kuyawasilisha kwenye Bodi ya Wadhamini wa

Mfuko wa Pembejeo kwa ajili ya kuidhinishwa.

B) Masherti ya Mkopo

- Waaombaji sharti wawe na dhamana isiyohamishika yenye hati miliki (Title deed) na inayokubalika kisheria. Mwombaji sharti awe ndiye mmiliki wa hati husika.

- Kadi za usajili za matrekta zitasajiliwa kwa pamoja na Mfuko na zitabaki kwenye Mfuko hadi mkopo wote utakapokuwa umerejeshwa.

- Muda wa mkopo ni miaka mitano kwa riba ya asilimia nane (8%).